**MULIKA Na. 39 2020 (159-168)**

# Changamoto za Tafsiri katika Enzi ya Utandawazi

Toboso Mahero na Mosol Kandagor[1]

Chuo Kikuu cha Moi, Kenya

**Ikisiri**

Ulimwengu unaendelea kuwa mdogo kwa sababu ya utandawazi. Katika muktadha wa lugha na fasihi ya Kiswahili, tunaweza kusema kuwa utandawazi umekuwa na athari kubwa kifasihi, kiisimu na kijamii. Ulimwengu wa sasa umeshuhudia ongezeko la matumizi mapana ya lugha anuwai za ulimwengu mbali na Kiingereza. Lugha kama Kiswahili, Kihindi, Kimandarin, Kichina, Kirusi, Kifaransa, Kiarabu na Kijapani zimeshuhudia ongezeko la matumizi yake kutokana na utandawazi. Kwa sababu hii, wafasiri na wakalimani walio na ujuzi katika lugha hizi wanahitajika katika maeneo anuwai ya ulimwengu. Hii ni kusema kuwa utandawazi umesababisha kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za tafsiri. Mbali na kupanuka kwa matumizi ya lugha, mahitaji haya pia yamesababishwa na teknolojia mpya ambayo imesababisha kupungua kwa gharama ya kubadilishana kwa ujumbe na matokeo ya tafiti. Changamoto za kisiasa ulimwenguni nazo zimesababisha haja ya kuwapo kwa wafasiri na wakalimani wengi katika kila pembe ya ulimwengu ili kushirikishwa katika michakato ya kutafuta amani na mapatano. Kwa sababu hii, changamoto anuwai zimezuka na kukumba wafasiri ikiwamo michakato ya tafsiri na vifaa vinavyotumika kutekeleza jukumu hili. Makala haya yanajadili changamoto zinazowakumba wafasiri katika michakato yao ya kutafsiri matini mbalimbali enzi au zama za sasa, zama za utandawazi.

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya utandawazi imefasiliwa kwa njia anuwai na wataalamu tofautitofauti. Chomsky (2006) anaifafanua kama hali ya kuleta utangamano wa kimataifa. Jones (2000) na Daly (1999) nao wanasema kwamba utandawazi ni umataifa na ubunaji wa soko moja la ulimwengu. Kwa hivyo, utandawazi ni mtindo wa mitagusano kati ya mataifa ya ulimwengu. Ni hali ya watu wa ulimwengu kuwa jamii moja, hali ambayo husababisha ukuaji wa mataifa kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia kutokana na kuathiriana na ulimwengu mpana. Kwa sababu hiyo, jambo linalotendeka katika nchi moja huathiri mataifa mengine ya ulimwengu. Katika utandawazi, miundo msingi ya kisiasa na mikakati ya kiuchumi huwa kitu kimoja. Mitagusano hii inahusu nyanja za

---

[1] Baruapepe: tobosomahero@gmail.com na markkandagor@gmail.com

kiteknolojia, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Chanzo cha mitagusano hii ni maendeleo katika mawasiliano, usafiri na miundo msingi. Mojawapo ya viashiria vya mifumo ya kiutandawazi ni kuenea kwa haja ya huduma za tafsiri pamoja na changamoto zake. Makala haya basi yanakusudia kujadili changamoto za tafsiri katika enzi za utandawazi, enzi ambazo mahitaji ya tafsiri ni makubwa sana.

Utandawazi umeathiri kwa kiasi kikubwa tafsiri pamoja na michakato inayohusiana na tendo la tafsiri. Athari ya utandawazi kwa tafsiri inatokana na hali ya utandawazi kusababisha ongezeko la mahitaji ya tafsiri ulimwenguni kote. Miongoni mwa mambo yaliyochochea kuongezeka kwa mahitaji ya tafsiri ni teknolojia mpya (Shiyab, 2010; Costales, 2011) na kuzuka kwa ruwaza mpya za tafsiri (Esselink, 2000; Schaffner, 2000). Teknolojia hii imesababisha kuenea kwa Kiingereza kama lugha kuu ya ulimwengu na hatimaye kusababisha ongezeko la mahitaji ya tafsiri. Shiyab anasisitiza kwamba kuenea kwa Kiingereza kumesababisha changamoto kwenye tafsiri katika maeneo mengi ya ulimwengu ikizingatiwa kwamba maandishi yaliyo katika lugha hii huhitajika kufanyiwa tafsiri ili kutumika katika maeneo ambamo Kiingereza kimeenea na ambayo yana lugha nyingine zinazotumika huko (Constales, 2011). Mathalani, Kiingereza si lugha asilia ya Afrika na Asia. Hii ina maana kwamba kuna lugha asilia zinazotumika katika maeneo hayo. Kwa sababu hii, maandishi yaliyo katika lugha hizi asilia huhitajika kutafsiriwa. Kadhalika, maandishi yaliyo katika Kiingereza huhitajika kutafsiriwa hadi katika lugha asilia za maeneo hayo. Hii ndiyo hali iliyosababisha kutafsiriwa kwa matini nyingi za Kiingereza kwa lugha ya Kiswahili, na pia kutoka Kiswahili kwa lugha ya Kiingereza. Kadhalika, hii ndiyo hali inayosababisha changamoto nyingi kwa wafasiri ikijumuisha michakato ya tafsiri na vifaa mbalimbali katika kutekeleza jukumu hili.

## 2.0 Changamoto kwa Vifaa vya Tafsiri

Katika muktadha wa utandawazi, vifaa vya tafsiri ni muhimu kutokana na nafasi inayotekelezwa na vifaa hivi katika mchakato wa tafsiri. Matumizi ya lugha nyingi za ulimwengu mbali na Kiingereza yamesababisha changamoto katika mchakato wa tafsiri. Vifaa asilia vya tafsiri vimepanuka kimatumizi na kusababisha changamoto anuwai (Constales, 2011; Schaffner, 2000; Corte, 2000; Esselink, 2000). Utandawazi umesababisha kupanuka kwa biashara za kimataifa na sasa mitandao inatumika zaidi katika mawasiliano ya kibiashara. Hali hii imesababisha kupanuka kwa taaluma ya tafsiri na kuleta changamoto kwa wafasiri na mchakato mzima wa tafsiri (Sandrini, 2005; Yunker, 2002; Crespo, 2008). Katika sehemu hii, tumetalii changamoto zinazokumba matumizi ya vifaa vya tafsiri na kuathiri michakato ya tafsiri.

### 2.1 Changamoto kwa Wafasiri Wasaidizi

Kuna aina mbili za wafasiri wasaidizi (Aspiration, 2008). Aina ya kwanza ni wafasiri wasaidizi wa kuhariri na ya pili ni wathibitishi. Wahariri hushughulikia miundo ya lugha na ubora wa tafsiri ilhali wathibitishi huwa na jukumu la kukosoa tafsiri kitahajia na kisarufi pamoja na kutazama urefu wa tafsiri yenyewe.

Katika enzi ya utandawazi, kuna tafsiri nyingi zinazofanywa kwa njia ya mtandao. Kupitia njia hii ya tafsiri, watu kutoka jamii na mataifa tofauti huhitaji huduma za tafsiri bila kuonana ana kwa ana. Kwa hivyo, wafasiri hutafuta mbinu za kushirikiana na wenzao kutoka mataifa mengine ili kutimiza mahitaji hayo. Katika kutekeleza jukumu hili, wafasiri na wasaidizi wao hukabiliwa na changamoto mbalimbali za kutafsiri matini. Makala haya yamebaini changamoto zifuatazo:

Changamoto ya kwanza ni ugumu wa kufahamu miktadha ya matini au maandishi. Suala la miktadha ya maandishi haliwezi kuepukika katika tafsiri (Baker, 2006; Pause, 1983, House, 2006 na Nida, 2001). Sababu ni kwamba matini nyingi huhusishwa na miktadha ya hali, wakati na mahali. Ni bayana kwamba matini ambayo ni usemi uliotolewa katika muktadha wa kisiasa itatofautiana na ile iliyotolewa katika mkutano wa mapatano, hata kama maneno yaliyotumiwa ni yaleyale. Hii ndiyo sababu utasikia mtu akikana ripoti kuhusu usemi wake na kusema kwamba nilieleweka vibaya. Kwa sababu hii, mtaalamu anayetafsiri matini kwa njia ya kidijiti hasa wakati huu wa utandawazi huhitajika kufahamu miktadha mbalimbali ili kuelewa maana ya matini asilia na kuweza kuihamisha hadi katika lugha pokezi.

Wafasiri na wasaidizi wao pia huhitajika kufahamu miktadha mbalimbali ya kimaandishi ili kufaulu katika kuhamisha ujumbe kamili uliomo katika matini. Wafasiri, kwa hivyo, huwa na changamoto ya kubainisha miktadha ya matini, hali ya mwandishi na wakati wa kuandikwa kwa matini asilia kabla ya kufanya tafsiri yake. Wafasiri hulazimika kusafiri hadi katika jamii za mwandishi ili kutafiti kuhusu miktadha ya matini zao. Changamoto huzuka katika harakati hizi za kutafiti kuhusu historia ya mwandishi ili kuelewa zaidi matini yake kabla ya kuitafsiri (Tong, 2001; Constales, 2010)

Utamaduni ni changamoto nyingine inayowakumba wafasiri wasaidizi. Ni muhimu kukumbuka kwamba utamaduni wa matini chanzi ni suala ambalo huathiri maana ya maandishi. Kwa hivyo, shughuli ya tafsiri huhitaji urazini wa utamaduni wa makala chanzi ili kutekeleza tafsiri iliyo bora. Utamaduni wa jamii huathiri moja kwa moja matumizi ya maneno na utunzi wa sentensi.

Lugha mwiko, kwa mfano, hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine, hali inayozaa tasfida ambazo zinahitaji kueleweka kwa wafasiri na wafasiri wasaidizi. Kadhalika, kuna misimbo ambayo huibuka kutokana na sheria za kitamaduni kuhusu matumizi ya lugha. Hali hii inashuhudia jinsi utamaduni ulivyo na athari kubwa kwa tafsiri. Hakika, wafasiri na wafasiri wasaidizi hawawezi kuepuka suala la kufahamu tamaduni za matini chanzi. Kwa hivyo, wafasiri na wasaidizi wao wanahitaji kuelewa utamaduni wa jamii nyingi za ulimwengu kwa kutegemea eneo na jamii ambamo matini wanazopata hutoka. Hii ndiyo sababu El-Dali (2011) aliwahi kusisitiza kwamba utamaduni wa lugha lengwa usilazimishwe kwa matini asilia. Anashikilia kwamba kila matini itazamwe kwa kuzingatia utamaduni wa matini na lugha asilia.

Ni muhimu pia kufahamu kwamba tamaduni za jamii hubadilika kutokana na wakati. Mathalani, tamthilia ya Antigoni iliyoandikwa na Sofokile karne nne kabla ya Kristo itafasiriwa na wafasiri wa sasa kwa kuzingatia utamaduni wa wakati wa Sofokile ambao ni tofauti na utamaduni wa Wagiriki wa wakati huu. Hali kama hii ndiyo hulazimu wafasiri kutafiti kuhusu utamaduni wa jamii ya mwandishi ili kufanikisha tafsiri yake. Mwandishi pia anaweza kukiuka utamaduni wa jamii yake anapoandika matini yake. Kwa hivyo, mfasiri sharti atafiti kuhusu utamaduni wa mwandishi mwenyewe pamoja na maisha yake. Tamaduni pia husambaa kutoka jamii moja hadi nyingine. Kwa mfano, baadhi ya tamaduni za jamii za Ulaya zimesambaa hadi katika jamii za Kiafrika. Tamaduni hizi zinajidhihirisha katika fasihi, dini, nyimbo, mavazi, elimu, lugha, siasa na sheria. Kwa sababu hii, wafasiri wana changamoto ya kubainisha maingiliano ya tamaduni wakati wa kutafsiri matini mbalimbali.

Wafasiri wasaidizi pia hukabiliwa na changamoto ya kidini. Utandawazi umesababisha kuenea kwa dini katika maeneo mengi ya ulimwengu. Kadhalika, watu wenye imani anuwai wamehamia katika maeneo tofautitofauti ya ulimwengu. Hali sasa ni tofauti na ilivyokuwa miaka ya zamani ambapo watu waliishi katika eneo finyu la jamii zao za asili. Usambaaji huu wa dini pamoja na uhamaji wa watu unasababisha changamoto za kidini kwa wafasiri na wasaidizi wao. Sababu ni kwamba imani za kidini huwa na athari kubwa kwa maana ya matini. Hii ndiyo sababu El-Dali (2011) aliwahi kutoa maoni kwamba matini chanzi yenye mungu wa kike itakuwa na tatizo la kuitafsiri iwapo mfasiri na wasaidizi wake wanatoka katika jamii yenye mungu wa kiume. Kadhalika, matini hiyo itakuwa na changamoto za tafsiri iwapo itatafsiriwa hadi katika utamaduni wenye mungu wa kiume hata ikiwa mfasiri anatoka katika utamaduni wenye mungu wa kike kama matini asilia. Changamoto kama hizi hulazimu wafasiri na wasaidizi wao kufanya uchunguzi na kuelewa miktadha ya kidini kabla ya kufanya tafsiri.

Ushirikiano pia huwa changamoto kubwa kwa wafasiri wasaidizi. Utandawazi unalazimisha ushirikiano kati ya wafasiri na wasaidizi walio katika maeneo tofauti ya ulimwengu. Hii inatokana na haja ya wafasiri kushirikiana na wahariri na wathibitishi walio na uzoefu au tajriba kubwa katika lugha zinazohusika. Utandawazi umesababisha hali ambapo wafasiri na wasaidizi wao wanalazimika kubadilishana maoni na wenzao kutoka maeneo mengine ili kufikia mwafaka kuhusu mielekeo mipya ya kitafsiri.

Suala la utamaduni na miktadha ya matini hulazimu ushirikiano wa wafasiri ili kurahisisha michakato ya tafsiri. Mfasiri anayetaka kutafsiri matini yasiyohusu jamii anamoishi hulazimika kutafuta na kushirikiana na wafasiri waliomo katika jamii ya mwandishi. Hata hivyo, ushirikiano kama huu unaweza kuwa ghali kwa kuwa unahitaji mawasiliano ya mara kwa mara, kusafiri, mikutano pamoja na makongamano. Mfasiri pia anaweza kukabiliwa na tatizo la ukosefu wa mfasiri mwenza kutoka katika jamii ya mwandishi wa matini asilia. Tatizo hili linaweza kuzuka iwapo mwandishi anatoka katika jamii ambayo haijawezeshwa kielimu na kiuchumi.

Kadhalika, wafasiri wasaidizi hukabiliwa na changamoto ya kiasi cha kazi. Umataifa wa ulimwengu umesababisha kuingiliana kwa mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya mataifa mbalimbali. Maingiliano haya humaanisha kuwa ili kupata huduma bora zaidi za tafsiri pana haja ya kuweka kandarasi, mapatano na hata haki za kunakili katika lugha mbalimbali za ulimwengu. Hali hii inawapa wahariri na wathibitishi kazi zaidi na hata kuhitaji wapate mafunzo yatakayowapa ujuzi zaidi katika taaluma yao na kupatiwa vifaa ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo. Katika nyanja za siasa, mitagusano imekuwa mingi kati ya mataifa na kusababisha kuongezeka kwa mahitaji ya tafsiri. Sekta ya afya pia imeathiriwa na utandawazi kutokana na watu kutoka mataifa mbalimbali kutafuta huduma za afya na ujuzi wa matibabu katika mataifa mengine. Hii imepelekea kuongezeka kwa haja ya tafsiri katika sekta hiyo. Ongezeko hili lina maana kwamba wafasiri na wasaidizi wao wanahitaji kufanya kazi zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya enzi za utandawazi.

Utandawazi umesababisha makampuni ya kibiashara kufungua biashara katika mataifa mengi ya ulimwengu. Makampuni yanayofungua matawi katika mataifa yasiyotumia lugha sawa na ile inayotumiwa katika mataifa ya makampuni hayo hulazimika kufanya tafsiri nyingi ili kufanikisha malengo yao. Kwa sababu hii, kuna ongezeko la kiasi cha tafsiri zinazofanywa ulimwenguni kote. Hali hii inamaanisha kwamba wafasiri wana kiasi kikubwa zaidi cha kazi ikilinganishwa na miaka iliyopita. Kwa mantiki hiyo, hata

kiwango chao cha ujuzi kitapaswa kiwe cha juu zaidi, jambo ambalo pia linazua changamoto kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

### 2.2 Changamoto za Ujuzi na Maarifa

Utandawazi umesababisha kusambaa kwa teknolojia mpya ya habari na mawasiliano ambayo imekuwa ala muhimu katika nyanja ya tafsiri. Kusambaa kwa teknolojia hii kumesababisha haja ya kuwapo kwa mafunzo zaidi kwa wafasiri, wasaidizi wao, wahariri na wathibitishi. Wafasiri hulazimika kujifundisha programu mpya za kompyuta pamoja na kujifunza matumizi ya mitambo mipya ya kufanikisha tafsiri. Kwa hivyo, wafasiri hukumbana na gharama kubwa ya kufanikisha elimu ya ziada ya kujiwezesha kiteknolojia. Gharama nayo huathiri uwezo wa kupata ujuzi zaidi kuhusu mchakato wa tafsiri.

Umataifa wa biashara umesababisha kupanuka kwa matumizi ya mitandao na vyombo vya habari vya kijamii. Katika mchakato huu, makampuni mbalimbali ya kibiashara hulazimika kutafsiri kurasa zao za mitandao hadi katika lugha nyingi ili kufikia na kufaidi wazungumzaji wa lugha nyingi. Kwa sababu hii, wafasiri na wasaidizi wao wamelazimika kupata ujuzi zaidi wa lugha na kufanya kazi zaidi. Wafasiri hujifunza lugha nyingi ili kupata uwezo wa kuelewa matini nyingi chanzi na hata kuelewa msamiati wa lugha anuwai ambao unaweza kuwa umetumiwa katika matini moja. Wafasiri hasa hufanya juhudi za kujifunza lugha kuu za ulimwengu kama Kifaransa, Kiingereza, Kijerumani, Kireno na Kiitaliano, na katika muktadha wa sasa wanapaswa pia kujifunza Kiswahili. Kwa maneno mengine, wafasiri wa Afrika pia hulazimika kujifunza Kiarabu, Kiswahili na Kiafrikana. Ujifunzaji wa lugha anuwai huwa na changamoto ya kufikia umilisi uliotukuka katika lugha zote husika. Ni muhimu kukumbuka kwamba mfasiri asiye na umilisi au ujuzi uliotukuka kuhusu lugha anazotafsiri anaweza kukabiliwa na changamoto katika kufanikisha tafsiri.

Ukuaji wa sekta ya elimu na utegemeanaji kati ya mataifa katika kutoa elimu kwa watu ni changamoto nyingine ya kimaarifa inayowakabili wafasiri. Katika enzi hii ya utandawazi, shule na vyuo vikuu katika mataifa mengi ya ulimwengu zimepanga mikakati ya kutegemeana katika kutoa elimu na mafunzo. Kutegemeana huku kumesababisha changamoto kwa wafasiri na wasaidizi wao kwa sababu ya tofauti katika lugha zinazotumiwa katika kutoa mafunzo. Mathalani, nchi nyingi zilizo katika jumuiya ya madola hutumia Kiingereza kama lugha rasmi na pia lugha ya mafunzo rasmi ilhali kuna nchi nyingine nyingi zinazotumia Kifaransa, Kijerumani na Kihispania. Lugha ya Kimandarin pia imeanza kusambaa kwa kasi ulimwenguni nje ya Uchina.

Athari mojawapo ni kwamba ushirikiano kati ya wafasiri na wasaidizi wao kutoka nchi zilizo na tofauti hizi za kilugha hukumbwa na matatizo ya kimawasiliano.

**2.3 Changamoto za Vifaa vya Tafsiri**

Uchunguzi uliofanywa pia umebaini kuwa kuna changamoto mbalimbali zinazowakabili wafasiri zinazotokana na vifaa vya tafsiri kama vile tarakilishi na kamusi. Mathalani, matumizi ya tarakilishi katika tafsiri yamekuja na changamoto tele kwa sababu ya utandawazi. Maingiliano kati ya watu yamesababisha mahitaji makubwa ya tafsiri katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mahitaji haya ndiyo yaliyosababisha uvumbuzi kuhusu matumizi ya tarakilishi katika tafsiri. Mtindo huu sasa unajulikana kama tafsri mashine. Hata hivyo, changamoto kubwa iliyopo ni kwamba mashine hizi hutegemea data ya ujozi-lugha ambayo hutokana na utafsiri wa wataalamu. Mashine zinazotumika katika tafsiri hupewa kamusi, vishazi, virai na sentensi za lugha mahususi kabla ya kuanza kutumika katika mchakato wa tafsiri. Kwa hivyo, sharti mashine hizo ziwezeshwe kidata ili kuwa na uwezo wa kutafsiri. Data hii huhitaji utafiti wa kina kuhusu lugha mbalimbali ili kutunga kamusi faafu za kuzipa mashine hizi uwezo. Kwa mfano, kuna lugha 7,117 ulimwenguni (Ethnolojia, 2020). Hata hivyo, ni lugha 42 pekee zilizo na data ya msamiati na sentensi katika mashine za kutafsiri (VentureBeat, 2016). Hii inazua changamoto kuhusu tafsiri ya lugha nyingine nyingi za ulimwenguni zinazotagusana na hivyo kuhitaji tafsiri. Hii pia inamaanisha kwamba mashine hizi hazina uwezo wa kufanya tafsiri zinazohusu lugha nyingi za ulimwengu ambazo hazina data katika mashine za kutafsiri. Mathalani, lugha nyingi za Kiafrika hazina data katika mashine za kutafsiri. Ingawaje lugha kama Kiingereza zina data katika mashine hizi, haiwezekani kufanya tafsiri inayoshirikisha Kiingereza na lugha nyingi za Kiafrika kwa kuwa mashine za kutafsiri hutegemea kuwapo kwa jozi za lugha ili kufanikisha tafsiri.

Changamoto hii inaweza kusuluhishwa kwa kuhakikisha kwamba kuna data ya kila lugha ya ulimwengu katika mashine za kutafsiri. Hata hivyo, changamoto nyingine inayoweza kuzuka hapa ni kwamba lugha nyingi hazijasanifishwa wala hazitumiki katika ufundishaji au mawasiliano mapana. Lugha nyingine zipo hatarini kupotea na hivyo, harakati za kutunga data katika lugha hizi zinaweza kukabiliwa na matatizo hasa iwapo juhudi hazitafanywa kuokoa lugha hizi.

Changamoto ya miundo ya lugha pia huwa nyeti kwa tarakilishi. Kwa mujibu wa Shirika la Milengo July (2013), jukumu la tarakilishi la kuhifadhi data kuhusu lugha na kutumia data hiyo katika tafsiri ni kubwa mno. Vilevile,

mashine za tarakilishi hazina uwezo wa kufikia ubora wa tafsiri kama ule wa wanadamu kutokana na changamoto za kufasiri miundo ya lugha. Robin (2009) anadai kwamba tafsiri mashine hukabiliwa na changamoto nyingi za kiisimu, hasa kutokana na miundo changamano isiyoweza kufasirika kwa mashine. Changamoto nyingine inatokana na ufasiri wa maneno. Anasisitiza kwamba siyo maneno yote ya lugha yana visawe katika lugha nyingine. Baadhi ya maneno katika lugha moja huenda yakahitaji kundi la maneno ili kueleza jambo moja. Kazi kama hii si rahisi kutekelezwa kwa kutumia tarakilishi. Lugha mbalimbali za ulimwengu zina miundo tofauti. Mathalani, miundo ya Kiswahili inatofautiana na ile ya lugha za Asia-Ulaya kama Kiingereza. Kwa sababu hii, mashine zinazofanya tafsiri zinaweza kukabiliwa na changamoto ya kufanikisha tafsiri inayohusisha Kiswahili na Kifaransa au Kiingereza.

Kadhalika, changamoto ya semantiki huathiri matumizi ya tarakilishi katika tafsiri. Katika lugha nyingi, neno moja linaweza kuwa na maana nyingi. Vilevile, sentensi moja inaweza kuwa na maana nyingi. Kwa hiyo, tafsiri mashine hupungukiwa katika kutafsiri sentensi na maneno kama haya. Vilevile, mchakato wa tafsiri huhitaji tajriba au ujuzi na uzoefu ambao mashine kama tarakilishi hazina. Tarakilishi hazina uwezo wa kutafakari kama ule wa mwanadamu. Kubadilika kwa lugha pia huathiri tafsiri ya sentensi kwa sababu lugha zote za ulimwengu hubadilika kulingana na wakati. Msamiati uliopo huzeeka na kutupiliwa mbali huku msamiati mwingine mpya ukizuka na kuanza kutumiwa. Katika hali hii, tafsiri ya tarakilishi hukabiliwa na upungufu iwapo hakutakuwa na juhudi za kufanya mabadiliko ili kuzifanya mashine hizo ziendane na miundo ya lugha zinazohusika.

Changamoto ya ubora wa tafsiri ni tatizo jingine linalokabili tarakilishi. Wafasiri wengi wanaotumia mashine hutumia programu ya *Microsoft* neno katika tafsiri yao. Hata hivyo, ubora wa tafsiri ya mashine haujafikia ubora wa tafsiri ya binadamu. Kwa sababu hii, vyombo vya habari vinavyotangaza au kuandika habari katika lugha zaidi ya moja hukumbwa na tatizo la ubora wa taarifa zao zilizofanyiwa tafsiri kwa njia ya mashine. Habari asilia huwa bora ilhali ile iliyotafsiriwa huwa na matatizo mengi ya kitafsiri. Baadhi huwa na changamoto za msamiati uliotumiwa vibaya au hata kuhifadhiwa kwa msamiati wa lugha asilia uliotumiwa katika makala asilia.

Mbali na changamoto zitokanazo na matumizi ya tarakilishi kama kifaa cha kufanyia tafsiri, pia kuna changamoto za matumizi ya kamusi. Uvumbuzi wa teknolojia mpya katika nyanja mbalimbali umekuwa changamoto kubwa kwa wafasiri. Ni muhimu kukumbuka kwamba uvumbuzi huu huandamana na msamiati wa kurejelea teknolojia husika. Aghalabu, msamiati ambao hubuniwa

kurejelea teknolojia mpya hufuata mofolojia ya lugha za wavumbuzi. Hii ina maana kwamba teknolojia mpya ikivumbuliwa na Wafaransa, basi teknolojia hiyo itapewa msamiati wa Kifaransa. Kwa sababu hii, watu wanaoagiza au kununua teknolojia hii hulazimika kujitokeza na msamiati faafu wa kutaja teknolojia hiyo katika lugha zao.

Katika jamii nyingi, jukumu hili huwa la wataalamu hasa wafasiri. Hii inaonyesha kwamba kutegemeana kwa mataifa kiteknolojoa huandamana na changamoto nyingi za kitafsiri. Changamoto za msamiati huzuka iwapo wataalamu wa tafsiri watachelewa kubuni msamiati wa kurejelea teknolojia hiyo mpya. Katika hali hii, kamusi zilizopo hukosa msamiati faafu wa kurejelea teknolojia hiyo. Hali hii ndiyo husababisha wazungumzaji wa lugha zinazopokea teknolojia hiyo kufanya juhudi za kubuni msamiati wao wa kurejelea teknolojia hiyo. Aghalabu, katika juhudi hizi msamiati mwingi huzuka kurejelea kitu kimoja.

Changamoto kwa kamusi hasa huwa kubwa katika hali ambapo teknolojia nyingi zinabuniwa kwa kasi kuliko juhudi za wataalamu za kubuni msamiati. Mathalani, katika uwanja wa mawasiliano, teknolojia nyingi zimekuwa zikizuka kila wakati. Teknolojia hizi zimekuwa za manufaa makubwa kwa jamii, kwa hivyo, husambaa kwa kasi mno na kuanza kutumiwa na wanajamii wengi ulimwenguni kote. Kusambaa kwa kasi kwa teknolojia hii husababisha pengo la ubunifu wa msamiati kwa kuwa wanajamii huanza kutumia teknolojia hii kabla ya wataalamu wa tafsiri kubuni au kuelewana kuhusu msamiati faafu wa kurejelea teknolojia husika.

## 3.0 Hitimisho

Imebainika katika makala haya kwamba ingawaje utandawazi umekuja na manufaa mengi kwa huduma za jamii ikiwamo utoaji wa huduma za tafsiri, kuna pia changamoto nyingi ambazo zimeandamana na manufaa hayo. Imebainika kwamba vifaa mbalimbali vya tafsiri vimekabiliwa na changamoto anuwai ambazo zimewalazimu wafasiri na wasaidizi wao kupanga mikakati ya kuyasuluhisha. Mikakati hii imekuwa na gharama ambayo wafasiri na wasaidizi wao wanalazimika kumudu ili kufanikisha kazi yao. Baadhi ya changamoto ambazo zimeibuliwa na utandawazi ni zile zinazotokana na tamaduni. Imebainika kwamba wafasiri na wasaidizi wao sharti wafahamu utamaduni wa matini asilia pamoja na waandishi wao ili kufanikisha tafsiri zao. Changamoto ya dini nayo inalazimu wafasiri kufanya utafiti kuhusu dini iliyoathiri matini asilia ili kuwasaidia kuelewa matini asilia. Changamoto nyingine ni zile zinazitokana na kuwapo kwa teknolijia mpya ambayo imekuwa ala muhimu katika mchakato wa tafsiri. Changamoto hizi zinasababisha hali

ambapo wafsairi na wasaidizi wao wanalazimika kujiandaa kifedha na kuhakikisha kwamba wanajihami na teknolojia mpya ya habari na mawasiliano. Vilevile, wafasiri wanatakiwa kupata mafunzo ya kila mara ili kuinua kiwango chao cha maarifa na ujuzi unaoendana na mabadiliko katika teknolojia mpya kuhusiana na utoaji wa huduma za tafsiri.

**Marejeleo**

Aspiration (2008). *Open Translation Tools: Disruptive Potential to Broaden Access to Knowledge.*

Chomsky, N. (2006). "Noam Chomsky chats with Washington Post Readers". Katika *The Washington Post,* imesomwa mtandaoni Machi 24, 2020.

Costales, A. F. (2011). "Translation 2.0: Facing the challenge of the global erra". *Linguistica Antverpiesia.* Toleo Jipya. Kur. 179-194.

Cronin, M. (2006). *Translation and Identity.* Washington: Taylor and Francis.

Daly, H. (1999). "Globalization vs Internationalization". Katika *Ecological Economics.* Juz. *3: 31-37.*

Eldali, H. (2011). "Towards an Understanding of the Distinctive Nature of Translation Studies". *Journal of King Sand University-Language and Translation.* Juz. Na. *23:* 29-45.

Mifflin, H. (2001). *The American Heritage Dictionary (Toleo la nne).* Boston: Tuitleback School & Library Binding Ltd.

Jones, B. R. (2000). *The World Turned Upside Down: Globalization and the Future of the State*. New York: St. Martins Press.

Mwansoko, H. J. M. Mekacha, R. D. K. na Masoko, D. L. W. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dares Salaam: TUKI.

Newmark, P. (1982). *Approaches to Translation.* Oxford: Pergamon.

Nida, E. A. na Taber, C. R. (1969). *The Theory of Translation*. London: Prentice Hall.

Robin, H. (2006). "Lost in Translation". Yamesomwa Mtandaoni katika www.bbc.co.ke>Drama>actionandadventure.

Steiner, G. (1975). *After Abel: Aspects of Language and Translation.* Oxford: Oxford University Press.

Wanjala, S. F. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa Ngazi ya Sekondari, Vyuo na Ndaki.* Mwanza: Serengeti Education Publishers.